



## **TAARIFA KWA UMMA**

### **WITO WA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA JKT KWA MUJIBU WA SHERIA MWAKA 2022 AWAMU YA PILI**

Mkuu wa Jeshi la Kujenga Taifa (JKT), Meja Jenerali Rajabu Mabele anawataka kuripoti Makambini Vijana wote walioitwa kuhudhuria Mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2022 ambao hawajaripoti mpaka sasa, Waripoti Makambi ya JKT mara moja.

Aidha, JKT limetoa nyongeza ya majina ya vijana waliohitimu elimu ya kidato cha sita

mwaka 2022 kujiunga na mafunzo ya JKT kwa Mujibu wa Sheria kwa mwaka 2022.

Vijana hao wote Waripoti Makambi ya JKT yaliyo karibu na maeneo wanayoishi, **Isipokuwa Kambi ya Makutupora JKT iliyopo Mkoani Dodoma, CUJKT iliyopo Kimbiji Mkoani Dar es Salaam na Ruvu JKT iliyopo Mlandizi Mkoani Pwani ambayo inapokea wahitimu wenye ulemavu wa kuonekana kwa macho (Physical Disabilities) yenye miundombinu ya kuwahudumia watu wa jamii hiyo.**

Vijana hao wote wanatakiwa kuripoti Makambi ya JKT kuanzia leo tarehe 22 Juni 2022 na mwisho wa kuripoti ni tarehe 25 Jun 2022.

Orodha kamili ya majina ya vijana walioitwa Awamu ya pili, Vifaa wanavyotakiwa kwenda navyo, Vipatikana katika tovuti ya JKT ambayo ni [www.jkt.go.tz](http://www.jkt.go.tz)

Mkuu wa JKT Meja Jenerali Rajabu Mabele, Anawakaribisha vijana wote walioitwa ili waweze kujiunga na vijana wenzao katika kujifunza Uzalendo, Umoja wa Kitaifa, Stadi za kazi, Stadi za Maisha na utayari wa kulijenga na kulitumikia Taifa.

  
Brig Gen

Imetolewa na:  
Kurugenzi ya Habari na Uhusiano,  
Makao Makuu ya JKT,  
Tarehe 22 Juni 2022.

